KASHUKA CHINI TOKA
KWENYE
UTUKUFU WAKE

JOE CREWS

KASHUKA CHINI TOKA KWENYE UTUKUFU WAKE

Na Joe Crews

(Hotuba ya Mambo ya Kweli ya Kushangaza)

Mfasiri: M. Mwamalumbili

Down From His Glory - Kiswahili

KASHUKA CHINI TOKA
KWENYE
UTUKUFU WAKE

Kifo chake Kristo alichokufa badala yetu pale msalabani kinasimama katikati ya kweli zile nyingine zote za wokovu ambazo zimefunuliwa katika Biblia. Alichukua mahali petu na kupata mateso ya adhambu ya dhambi zetu. Madai ya Sheria [Amri Kumi] dhidi ya mvunjaji wa Sheria hiyo [Amri Kumi] yalitoshelezwa kabisa kwa njia ya yeye kuikubali kwa hiari yake adhabu ile iliyokuwa yetu. Kuupotosha ukweli huo mkuu sana unaohusu Mpango wa Wokovu ingekuwa ni kuudhofisha msingi mzima wa Ukristo. Ni kweli hii kuu sana ya Biblia inayohusu wema wake Kristo ambao tulipewa kwa njia ya upatanisho wa kifo chake kinachompa dhamana kila muumini aliyezaliwa mara ya pili.

Daima limekuwa ni kusudi lake Shetani kuufunika ukweli huo rahisi wa msalaba unapotumika kulitatua tatizo letu la dhambi. Katika vipindi mbalimbali vya historia, amezusha maswali mengi yaletayo utata kuhusu aina ya kafara aliyoitoa Kristo pale msalabani. Kumbukumbu za mwanzo za Kikristo huonyesha kwamba yalikuwako makundi fulani ambayo hayakusadiki kwamba Bwana wetu alikuwa ni Mungu kamili. Waariani (Arians), kwa mfano, walifundisha kwamba Yesu alikuwa ni kiumbe tu kilichoumbwa. Shule nyingine ya theolojia ilisadiki kwamba kifo cha Yesu kilikuwa ni mwonekano tu ambao haukuambatana na kuyakatisha kabisa maisha yake kwa kifo [yaani, alionekana tu kama amekufa, lakini hakufa kabisa]. Nadharia nyingi zinazogongana zenyewe kwa zenyewe zimezusha maswali mengi juu ya falsafa ya kanuni za upatanisho wake. Je, angewezaje kuchukua maovu yetu na kuikubali adhabu yetu kwa njia ambayo inatufanya sisi kutangazwa kwamba tuna haki, wala hatuhukumiwi?

Biblia inafundisha kwamba Kristo "alidhihirishwa katika mwili" [1 Tim. 3:16] kwa kusudi la kutimiza mambo fulani kwa ajili ya ukombozi wa wanadamu. Kwanza kabisa, angepaswa kuishi maisha ya utii kamili [kwa Amri Kumi – Yn. 15:10] ili kufidia kule kushindwa kwa mwanadamu. Pili, angehitaji kuichukua yeye mwenyewe dhambi ya mwanadamu iliyosababishwa na kuivunja Sheria [Amri Kumi – 1 Yoh. 3:4, AJKK] na kupata adhabu ya mauti [ya pili – Ufu. 20:14] iliyotakiwa na hiyo Sheria [Amri Kumi – Rum. 6:23a]. Mambo hayo mawili - yaani, kifo chake kilichoilipa fidia ya dhambi zetu, pamoja na utii wake mkamilifu [kwa zile Amri Kumi] - yangeweza kuhesabiwa kwa wale wote ambao wangempokea Yesu kama Badala yao aliye mtakatifu. Kwa imani, mwenye dhambi angeweza kuhesabiwa kwamba ameilipa ile adhabu ya mauti [ya pili] na kwamba ameishi maisha ya utii kamili [kwa zile Amri Kumi]. Uzoefu huo wa maisha, uitwao KUHESABIWA HAKI KWA IMANI, ndicho kitovu cha mafundisho ya Waprotestanti wote kuhusu wokovu. Kulingana na hilo fundisho zuri la Biblia, mwenye dhambi aliyetubu sasa anasimama mbele zake Mungu kana kwamba ni yeye mwenyewe aliyeitimiza adhabu ile. Wakati uo huo, kumbukumbu yake ile ya zamani ya kushindwa kwake na kuivunja ile Sheria [Amri Kumi] inafunikwa na sifa ile ya Kristo ya utii wake kamili [kwa zile Amri Kumi], ili aweze kuhesabiwa kama ana haki - yaani, kana kwamba alikuwa hajapata kamwe kutenda dhambi.

Fundisho lo lote linaloondoa tendo hilo la ajabu, ambalo linaleta mabadiliko katika maisha yetu, halina budi kufikiriwa kuwa ni uzushi wa hatari mno. Fundisho lo lote la dini ambalo lingefanya isiwezekane kabisa kwa Kristo kuishi maisha hayo makamilifu katika mwili [wa kibinadamu], au isiwezekane kwake kufa badala ya mwanadamu ni lazima lifikiriwe kuwa limekuwa adui wa haki.

Ningependa kudokeza kwamba mamilioni ya Wakristo hivi leo, bila ya wao kujua, wameukubali msimamo wa kitheolojia unaofanya jambo lilo hilo nililoongelea habari zake. Wengi sana miongoni mwa wale waliodanganywa katika jambo hilo wanaamini kabisa kabisa kwamba wanamheshimu Kristo kwa kuushikilia mtazamo wao huo.

Ni Ubinadamu Wa Aina Gani Ulitakiwa?

Kulielewa tatizo hilo, inatupasa kuangalia kwa undani sana somo hili la Kristo Kufanyika Mwili [Yn. 1:14]. Ilikuwa ni kule kuingia kwa Mwokozi wetu katika familia ya kibinadamu ambako kuliuweka msingi wa hatua zote za Mpango ule wa Ukombozi wetu. Kwa mujibu wa Maandiko, alipaswa kuzaliwa na mwanamke bikira, alipaswa kuishi maisha yasiyo na dhambi, na kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Je, ni kwa njia na umbile gani alitimiza matakwa yale? Ili kuitwaa asili [mwili] ya kibinadamu, alitakiwa kuchagua kati ya mbili tu zilizokuwapo - tabia takatifu, isiyoanguka dhambini aliyokuwa nayo Adamu kabla ya kuanguka kwake, au asili [mwili] iliyoanguka dhambini waliyokuwa nayo wazao wote wa Adamu. Endapo angeitwaa ya aina nyingine iwayo yote, basi, isingekuwa ni asili [mwili] ya kibinadamu hata kidogo.

Ulimwengu wa Kikristo leo umegawanyika juu ya jambo hili lihusulo asili [mwili] aliyoichagua Yesu kwa maisha yake alipofanyika mwili [Yn. 1:14]. Wale wanaosadiki kwamba alitwaa asili [mwili] ya Adamu kabla hajaanguka, yaani, kwamba alitwaa asili [mwili] isiyo na dhambi aliyokuwa nayo adamu kabla ya kuingia dhambini, wanaitwa Washabiki wa Msimamo Usemao kwamba Yesu Alitwa Asili [Mwili] ya Adamu KABLA ya Anguko (Prelapsarians). Wale wanaoamini kwamba Yesu alitwaa asili [mwili] ya mwanadamu iliyoanguka [dhambini] wanaitwa Washabiki wa Msimamo Usemao kwamba Yesu Alitwaa Asili [Mwili] ya Adamu BAADA ya Anguko (Prolapsarians). Haidhuru ni msimamo upi ambao mtu anauchagua katika kuafikiana na makundi hayo mawili, atakuwa amefungwa katika mipaka iliyowekwa na uchaguzi wake.

Hebu kwanza na tufikirie athari zinazoletwa na kuamini kwamba Yesu alikuja katika asili [mwili] ya Adamu isiyoanguka dhambini. Ni jambo linalochanganya sana mawazo kuweza kujua msimamo huo unatupeleka wapi. Kwanza kabisa, hebu na tuulize swali kwamba Adamu alikuwa na asili [mwili] gani kabla ya anguko lake. Naam, ilikuwa ni asili [mwili] kamilifu, inayotii [Amri Kumi za Mungu], ambayo dhambi haikuwa na ushawishi wo wote juu yake. Lakini ilikuwa ni zaidi ya hayo. Asili [mwili] ya Adamu kabla ya anguko pia ilikuwa ina uzima wa milele uliowekewa masharti, jambo ambalo linamaanisha kwamba asingeweza kufa, isipokuwa kwa kuchagua dhambi.

Ukweli ni kwamba hapakuwa na njia yo yote kwa Adamu asiyeanguka dhambini kuweza kuonja mauti, isipokuwa kwa njia ya kuacha kutii [zile Amri Kumi]. ASILI [MWILI] YA ADAMU ISIYOANGUKA DHAMBINI ISINGEWEZA KUFA. Ilikuwa katika hatari ya kufa wakati ule tu Adamu alipokuwa ametenda dhambi. Kama angekuwa hajatenda dhambi kabisa, basi, Adamu angekuwa ameendelea kula matunda ya ule mti wa uzima. "Utii, kamili na wa kudumu [kwa zile Amri Kumi], lilikuwa ndilo sharti la kuwa na furaha milele. Kwa sharti hilo alipaswa kuuendea ule mti wa uzima." Patriarchs and Prophets, uk. 49.

Mungu alipomwumba mwanadamu, alimwekea sharti ambalo kwalo angeweza kuishi milele. "Siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika" (Mwanzo 2;17). Mauti na kutengwa mbali na mti ule wa uzima ilikuwa ndiyo hukumu iliyotolewa dhidi ya mwanadamu yule kwa sharti pekee la kutenda dhambi. Kadiri Adamu na Hawa walivyoendelea kumtii Mungu, hawakuweza kula matunda ya mti ule, nao walikuwa hawawezi kupatwa na mauti. "Kama vile Adamu alivyoweza kuwa na hakika, muda mfupi tu kabla ya anguko lake, ya kuwa na uzima wa milele aliopewa na mti ule wa

uzima, ndivyo, sasa, kufuatia mkasa wake ule, kifo chake vile vile kilivyokuwa ni cha hakika." 1 BC, uk. 225.

Ni jambo la maana sana kwetu kuijua sababu iliyomfanya Yesu kuchukua mwili wa kibinadamu alipokuja hapa duniani. Biblia inasema, "Ila twamwona Yesu, aliyefanywa mdogo punde kuliko malaika, KWA SABABU YA MAUMIVU YA MAUTI [YA PILI] … ili kwa neema ya Mungu AIONJE MAUTI [YA PILI – Ufu. 20:14] KWA AJILI YA KILA MTU" (Waebrania 2:9, KJV).

Ilimpasa Yesu kuja kama mwanadamu ili KUIONJA MAUTI [ya pili ambayo ndiyo mshahara wa dhambi – Rum. 6:23a; Ufu. 20:12-15], NA KULIPA FIDIA YA DHAMBI ZETU. Ilimpasa kutwaa asili [mwili] ile iliyokuwa na uwezekano wa kufa. Lakini hapa ndipo ipo ile kweli inayoshangaza sana: Kama angekuwa amechukua ile asili ya Adamu isiyoanguka dhambini, basi, ASINGEWEZA KABISA KUFA [Eze. 18:20], ISIPOKUWA KAMA [YEYE MWENYEWE] ANGETENDA DHAMBI! Asili [mwili] ile ilikuwa haiwezi kukabiliwa na mauti mpaka pale ilipokuwa imedhoofishwa na dhambi. Yesu angeweza kuionja mauti tu kwa kuzaliwa katika familia iliyoanguka [dhambini] ya wazao wa Adamu. Kama alivyoandika mwandishi mmoja, "Kristo aliunganisha kweli asili [mwili] ile ya dhambi na asili [mwili] yake mwenyewe isiyo na dhambi, kwa sababu kwa tendo hilo la kujidhili, angeweza kuimwaga damu yake kwa ajili ya wanadamu walioanguka [dhambini]." EGW, Manuscript 166, 1898.

Ubinadamu Wake
Ulikuwa Katika Hatari ya Kufa

Paulo alilikazia sana jambo hilo alipoeleza jinsi Yesu alivyo"onekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti [kwa zile Amri Kumi – Yn. 15:10; Kut. 20:3-17], naam, mauti ya msalaba" (Wafilipi 2:8). Zingatia ya kwamba ilikuwa ni wakati ule tu alipoonekana ana umbo kama mwanadamu ndipo aliweza kuwa "mtii [kwa zile Amri Kumi] hata mauti" [yaani, mpaka kufa kwake]. UUNGU WAKE ULIKUWA HAUWEZI KUFA, kwa hiyo, asingeweza kuishi hapa na kufa kama Mungu. Ilimpasa kutwaa asili [mwili] ile ambayo ingeweza kufa. Upatanisho kwa ajili ya dhambi ungekuwa hauwezekani kabisa kufanyika kama yeye angezaliwa na asili [mwili] ile ambayo peke yake ingemwezesha kuwa "mtii hata mauti" [kwa zile Amri Kumi]," yaani, kama angekuwa na asili [mwili] ile aliyokuwa nayo Adamu kabla hajaanguka dhambini. Hii ndiyo maana Maandiko pia yanafundisha, yanasema, "Maana ni hakika, hatwai asili [mwili] ya malaika, ila atwaa asili [mwili] ya MZAO WA IBRAHIMU" (Waebrania 2:16).

Kwa nini hakuja na asili [mwili] ile ya malaika? Kwa sababu wao, kama Adamu, walikuwa wameumbwa wakiwa na uzima wa milele uliotolewa kwao kwa masharti, nao hawakuwa katika hatari yo yote ya kufa, isipokuwa tu au mpaka pale walipotenda dhambi. Kristo asingeweza kulipa fidia ya dhambi akiwa kama malaika, kwa sababu asingeweza kufa. Wala asingeweza kufanya upatanisho huo akiwa kama Adamu alivyokuwa kabla ya kuanguka kwake dhambini, kwa sababu asingeweza pia kufa katika asili [mwili] ile. Alikuwa hana budi kuja kama "mzao wa Ibrahimu."

Uzao wa Ibrahimu uliwajumuisha peke yao wale wote waliokuwa katika hatari ya kufa kutokana na dhambi ya Adamu. Endapo Kristo angalitwaa asili [mwili] ya Adamu kabla ya anguko lake, basi, asingeweza kabisa kupata maumivu ya mauti [ile ya pili] yaliyotakiwa kwa ajili ya dhambi zetu, isipokuwa tu kama yeye mwenyewe alikuwa ametenda dhambi kwanza, hapo dhambi ile ingemfanya asiwe na sifa inayotakiwa ya kuwa Mwokozi wetu.

Nasema tena kwamba hapa sisi tumefungwa katika mipaka inayotakiwa na asili [mwili] ile aliyokuwa nayo Adamu kabla ya kuanguka dhambini. Yesu alisema waziwazi kabisa kwamba yeye alikuwa anajitoa kuishi kama mwanadamu katika dunia hii, wala sio kama Mungu. Kwa kujifunga

mwenyewe katika hali ya kibinadamu, Yesu angeweza kupata kutoka kwa Baba yake NGUVU ZILE TU PAMOJA NA MANUFAA YALE TU AMBAYO WENGINE WANAOISHI KATIKA MWILI HUU WANAWEZA KUPATA. Tena na tena Kristo alisema kwamba yeye asingeweza kusema neno lo lote, wala kufanya lo lote ambalo alikuwa hajapewa na Baba yake [Yn. 14:21-24; 16:25].

Kwa maneno mengine, Yesu hakubadilisha mwelekeo wake kwenda upande huu au upande ule kati ya asili [mwili] yake ile ya Uungu na ile ya kibinadamu ili kuzikwepa shida za maisha haya ya duniani zinazohitaji kushughulikiwa upesi. Alikubali hatari, kukataliwa na watu kwa dharau, na kuteseka kutokana na kuishi maisha yake kama mwanadamu. Shetani kila wakati alijitahidi sana KUMCHOCHEA ATUMIE UUNGU WAKE ili kujiokoa mwenyewe kutoka katika hali fulani fulani, na hapana budi hilo lilikuwa ni jaribio [mtihani] lenye nguvu mno lililomkabili Bwana wetu kwa kutotumia uwezo wake mwenyewe [wa uungu] usio na kikomo wakati wa saa zile za mwisho za mateso yake makali sana katika maisha yake hapa duniani. Endapo angalikuwa amefanya hivyo, basi, Mpango ule wa Wokovu ungekuwa umeshindikana kabisa. Hata wakati wa kufa kwake, ilimpasa kujiweka chini ya hali zile alizowekewa na asili [mwili] yake ya kibinadamu.

Asili Ile Kabla ya Anguko
Isingeweza Kufa

Sasa tumefikishwa kwenye njia panda (dilemma). Ikiwa Yesu alikuwa na asili [mwili] ya Adamu aliyokuwa nayo kabla ya anguko lake, basi, ilikuwa haiwezekani kwake kufa, isipokuwa kwa KUTENDA DHAMBI yeye mwenyewe, au kwa KUZIBADILISHA KANUNI zile [Amri Kumi – Mt. 5:17-48; Lk. 16:17; Isa. 42:21] alizokuwa amekubali kuishi chini yake wakati wa maisha yake hapa duniani [Yn. 15:10]. Kwa kufanya mojawapo la mambo hayo mawili, Mpango ule wa Wokovu ungekuwa umeshindikana kabisa. Wengine wanaweza kudokeza kwamba kwa kuchukua dhambi ya mwanadamu na kufanywa dhambi kwa ajili yetu, asili [mwili] ya Yesu ilibadilishwa pia ili ipate kuionja mauti. Lakini hivyo sivyo lilivyo jambo hilo. Tendo lile la yeye kuchukua dhambi zetu kwa niaba yetu lisingeweza kuibadilisha asili [mwili] yake ya kibinadamu. Dhambi haikuingia katika maisha yake ili kumfanya awe mwovu au kumchafua. Yeye alizichukua dhambi zile tu kwa niaba yetu, jambo ambalo linamaanisha kwamba alizichukua KANA KWAMBA zilikuwa zake, japokuwa hazikuwa zake.

Lakini tafadhali zingatia sana tofauti hii muhimu: Alipotwaa asili [mwili] ya kibinadamu, hakufanya vile kwa niaba yetu. Hakuishi hapa KANA KWAMBA alikuwa mwanadamu. Aliitwaa kabisa kabisa asili [mwili] ya kibinadamu. Akawa mmoja wetu [mwenzetu/kaka yetu] kabisa [Isa. 9:6; 7:14,15; Ebr. 2:14-18; 4:15]. Kwa hiyo, kule kuzichukua mwilini mwake dhambi za mwanadamu hakukuyaathiri maisha yake, wala kuifanya asili [mwili] yake kuwa na uovu kana kwamba alikuwa ametenda dhambi halisi. Haidhuru ni asili [mwili] gani aliyokuwa nayo kwa miaka ile thelathini na mitatu, bado yeye aliendelea kuwa nayo, tena alikwenda nayo msalabani. Alikuwa mtakatifu baada ya kuzichukua dhambi zetu sawasawa tu na vile alivyokuwa mtakatifu kabla ya kuzichukua. Badiliko peke yake lilikuwa ni namna Mungu alivyomwangalia na kumshughulikia kisheria [kulingana na Amri Kumi – Yak. 2:10-12].

Kwa mujibu wa amri ya Mungu ya uumbaji, hali ile ya mwanadamu isiyokufa [uzima wa milele] ingeweza kupotezwa TU kwa KUTENDA dhambi. Isingeweza kupotezwa kwa njia fulani ya KUIHESABIA juu ya mtu aliyeichukua dhambi ile kwa niaba ya mwingine. Ni mvuto wa dhambi ule tu unaonajisi ambao unaingia moyoni mwa mtu ndio ungeweza kuleta badiliko la asili [mwili] yake ambalo lingemfanya mtu yule akabiliwe na hatari ya kifo [Mt. 15:19,20]. Jambo hilo halikutokea kabisa kwa Yesu. Kule kuhesabiwa kwake kuwa ana dhambi hakukumfanya awe na dhambi [2 Kor.

5:21]. Lakini basi, ile asili [mwili] yake ya kibinadamu *haikuhesabiwa* tu kwake: ilikuwa ni asili halisi kabisa. Naye ilimpasa kuukubali ukweli ule katika maisha yake yote, hata katika kuionja mauti pale msalabani. Ukweli kwamba alikubali kukabiliwa na mauti ile ni ushahidi thabiti unaoonyesha kwamba alikuwa hatendi mambo yake kulingana na matakwa ya asili [mwili] ile aliyokuwa nayo Adamu kabla ya anguko.

Wengine wanadai kwamba haileti tofauti yo yote kuhusu kile tunachokiamini juu ya suala hili la asili [mwili] ya Kristo alipofanyika mwili, lakini ukweli ni kwamba mambo makubwa mno yanategemea suala hili [1 Yoh. 4:1-6]. Endapo mimi nachagua kuamini kwamba Yesu alikuja katika asili [mwili] ile aliyokuwa nayo Adamu kabla hajaanguka dhambini, basi, kwangu hakuna njia yo yote ya kuniwezesha kukwepa mojawapo ya maamuzi haya yafuatayo:

(1) Asingeweza kufa ili kulipa fidia ya dhambi zangu, au
(2) Yeye mwenyewe, basi, alitenda dhambi ili kuweza kukabiliwa na kifo kile, au
(3) Alilazimika kutumia uwezo wake wa Uungu kuigeuza asili [mwili] ya kibinadamu aliyokuwa ameitwaa, ili kuondokana na mipaka iliyowekwa nayo. Ni kwa njia hiyo tu yeye angeweza kukabiliwa na mauti iliyohitajika kwa ajili ya ule upatanisho. Asili ile isiyoanguka dhambini isingeweza kufa.

Lo lote kati ya mambo hayo matatu yangekuwa yameuzuia kabisa uwezo wake wa kutimiza sehemu yake ya kuwa Badala yetu kama Mkombozi wetu.

Madai yametolewa kwamba wale wanaofuata fundisho lisemalo kwamba asili [mwili] ya Kristo aliyokuwa nayo ni ile aliyokuwa nayo Adamu baada ya anguko lake kwa njia hiyo wanamfanya yeye awe na hatia ya dhambi. Ningependa kutoa maoni yangu kwamba ni wale tu wanaoamini kwamba alikuwa na asili [mwili] ile aliyokuwa nayo Adamu kabla ya anguko ndio walio na mtazamo potofu. Kusema kweli, mtazamo wao ndio msimamo wa pekee unaomfanya Kristo atende dhambi ili kuweza kuutekeleza Mpango huo wa Wokovu.

Washabiki wa msimamo usemao kwamba Yesu alikuwa na asili [mwili] ile aliyokuwa nayo Adamu kabla ya Anguko (Prelapsarians) kwa unyofu wa moyo wanaamini kwamba kuzaliwa na asili [mwili] ile aliyokuwa nayo Adamu baada ya Anguko kungemfanya Yesu awe na hatia ya dhambi. Kwa sababu hiyo, katika jaribio lao linaloshindwa kabisa la kutaka kumwondoa katika hali ile inayomfanya akabiliwe na dhambi, wanamwondoa kutoka katika hali ile ya kukabiliwa na mauti!

Dhambi ya Asili Sio Fundisho la Biblia

Mbona basi, wale wanaoamini kwamba Yesu Kristo alikuwa na asili [mwili] ile aliyokuwa nayo Adamu baada ya Anguko wanashtakiwa kwamba wanamfanya Kristo kuwa mwenye dhambi? Hiyo ni kwa sababu tu wale wanaotoa shtaka hilo wanaamini katika fundisho la Dhambi ya Asili (Original Sin). Washabiki wa msimamo usemao kwamba Yesu alitwaa asili [mwili] ile aliyokuwa nayo Adamu baada ya Anguko HAWAAMINI KWAMBA TUNAHESABIWA DHAMBI KUTOKANA NA ASILI [MWILI] YETU, bali KWA UCHAGUZI WETU. Wao wanashikilia msimamo usemao kwamba Yesu hakuwa na dhambi yo yote alipozaliwa kama mwanadamu. Yeye alirithi tu asili [mwili] ile ile iliyodhoofika ambayo dhambi ilikuwa imeiweka juu ya wazao wote wa Adamu, lakini yeye hakuanguka chini ya udhaifu ule hata mara moja [Rum. 5:12,17,18]. Maisha yake yalikuwa matakatifu kabisa, wala hayakuwa na dhambi yo yote. Akiwa amejazwa na Roho Mtakatifu toka tumboni mwa mama yake, huku akitegemea kupewa nguvu kutoka mbinguni kila siku, aliishi maisha ya ushindi unaoendelea daima dhidi ya kila dhambi.

Maisha yale yale ya ushindi unaoendelea daima yanatolewa kwa kila mzao mwingine wa Adamu kupitia katika hatua zile za kuongoka na utakaso. Yesu alichagua kitu fulani tu kabla ya kuzaliwa

kwake ambacho sisi tunaweza kukichagua tu baada ya kuzaliwa kwetu. Yeye alichagua kuyasalimisha kabisa kwa Baba yake maisha yake ya kibinadamu tangu dakika ile mimba yake ilipotungwa. Sisi tunafanya uamuzi wetu huo wakati ule wa kuongoka kwetu, ndipo tunaanza kuwa washirika wa ile asili ya uungu ya Mungu - asili ile ile iliyomtegemeza Yesu kwa miaka ile thelathini na mitatu ya kuishi kwake hapa maisha yake matakatifu.

Tunafikishwa kwenye hitimisho lisilokanushika lisemalo kwamba somo hili si somo ambalo tunaweza kuchagua kutosimama upande wo wote. Katika fundisho lile la dini lisemalo kwamba Kristo alikuwa na asili [mwili] ile aliyokuwa nayo Adamu kabla ya Anguko, hatupotezi tu kutiwa moyo kwa kukosa kuuona mfano hata mmoja wa ushindi dhidi ya dhambi katika mwili kama huo, lakini pia tunafutilia mbali kuwapo kwa uwezekano wo wote kwa Kristo kuwa mchukuzi mtakatifu wa dhambi zetu. Mungu na apishe mbali, sisi tusilifedheheshe jina lake kwa kushikilia mtazamo huo finyu wenye makosa kuhusu kifo chake kile alichokufa badala yetu ambacho kinatuletea sisi upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu.

Wengine wametoa mchango wao kwa kutoa wazo lisemalo kwamba Yesu hakutwaa asili [mwili] ya Adamu aliyokuwa nayo kabla ya Anguko, wala ile aliyokuwa nayo baada ya Anguko la mwanadamu, yaani, kwamba alikuwa na asili [mwili] ya pekee kabisa ambayo wanadamu wengine wote hawakupata kuwa nayo. Wao wanapendekeza kwamba alikuwa na **asili ya kiroho** ambayo Adamu alikuwa nayo kabla ya Anguko ambayo ilikuwa imeunganishwa pamoja na **asili ya kimwili** aliyokuwa nayo Adamu baada ya Anguko. Wanaona kwamba ni lazima wafanye hivyo ili kuweza kutoa maelezo kuhusu maisha ya Yesu yasiyokuwa na dhambi ambayo alikuwa nayo katika miaka ile ya utoto na ujana wake. Lakini, je! hivi ni lazima kumpa asili iliyo tofauti kabisa kwa sababu yeye alikuwa na uzoefu wa maisha ulio tofauti na watoto wengine? Hivi maisha yake yalitofautianaje na yao? Yake yalikuwa ni maisha ya kujisalimisha kabisa na kumtii Baba yake [Zab. 40:7,8; Ebr. 10:5-7,10; Yn. 15:10]. Je, maisha hayo wanaweza kuwa nayo watoto wengine? Ndiyo, wanaweza, wanapokuwa wamekua kiasi cha kutosha kuweza kujitoa kabisa wenyewe kwa Kristo. Kwa kuwa yeye alikuwako milele kabla yetu, aliweza kujitoa kabla hajazaliwa. Ikiwa wanadamu wengine wanaweza kuutumia uwezo ule unaowapatia ushindi dhidi ya dhambi baadaye wanapokuwa wamefikia umri mkubwa zaidi, licha ya wao kuwa na ile asili [mwili] iliyoanguka dhambini, kwa nini, basi, Yesu asingeweza kufanya vivyo hivyo wakati ule alipokuwa na umri mdogo sana - akiwa na asili [mwili] ile ile waliyo nayo wao? Hapa tunazungumzia tu juu ya TOFAUTI YA UMRI, sio juu ya asili [mwili] yao.

Mtu fulani mmoja anaweza kusema hivi, Vema, hilo linampa Yesu nafasi nzuri sana ya kujiendeleza kiroho kuliko sisi." Lakini, ngoja kidogo. Ni nafasi nzuri gani hiyo? Kama wewe ulimpokea Kristo miaka miwili kabla mimi sijafanya hivyo, basi, wewe ulikuwa na nafasi nzuri kuliko mimi ya kukua kiroho KATIKA KIPINDI CHA MIAKA ILE MIWILI. Ukweli ni kwamba Kristo alikuwa na nafasi nzuri zile zile kuliko sisi ambazo nasi tunazo dhidi ya wengine wote wanaoingia katika uzoefu wa kuongoka baadaye sana kuliko sisi. Tofauti hiyo haiko katika asili [mwili] yetu tuliyo nayo, ila ni jambo tu lililo la kawaida kwa kila mtu anayejitoa maisha yake yote kwa Kristo bila kuacha kitu. Kwa maneno haya sisemi kwamba Yesu alihitaji kuongoka au aliongoka baada ya kuzaliwa kwake. Yeye alijazwa Roho Mtakatifu toka tumboni mwa mama yake, kwa hiyo maisha yake ya kutokuwa na dhambi msingi wake ulijengwa juu ya kitu fulani ambacho sisi tunaweza tu kukionja wakati ule tunapozaliwa mara ya pili.

Ukinzani ni upi, basi, dhidi ya kuamini kwamba Yesu alikuwa na asili ya kiroho ambayo Adamu alikuwa nayo kabla ya Anguko lake ambayo iliunganishwa na asili ya kimwili aliyokuwa nayo Adamu baada ya Anguko? Makosa mazito matatu yanaonekana kuifanya imani hiyo kutopatana kabisa na theolojia ya Biblia.

(1)
Inagongana Vibaya na Mtazamo Mzima
Wa Biblia Juu ya Asili [Mwili] ya Mwanadamu

Ni wapi ambapo Biblia inafundisha kwamba mwili na roho vimegawanyika katika sehemu mbili tofauti? Ukweli wa Maandiko sikuzote umeunga mkono ufahamu ule unaoiunganisha asili [mwili] ya mwanadamu kuwa ni kitu kimoja, mwili na roho vikiingiliana pamoja hufanya kazi yao ili kuleta afya kamili kiakili na kimwili. Lakini basi, tunapokuja kwenye asili [mwili] ya Kristo wazo hilo la kuiangalia kwa jumla asili hiyo linatupiliwa mbali, ndipo wengine huanza kuongea katika lugha inayozipambanua sehemu mbili zilizo tofauti, sehemu moja ya asili ya Kristo ikiwa na dhambi na sehemu nyingine ikiwa haina dhambi.

Je, hivi ingewezekanaje kuwamo mwungano kama huo ndani yake [Yesu] ambao unaiunganisha asili ile ya kiroho aliyokuwa nayo Adamu kabla ya Anguko lake na asili yake ya kimwili aliyokuwa nayo baada ya Anguko, ambayo wanayo wanadamu wote wenye dhambi? [Rum. 3:23; 5:12.] Je, hivi sisi tunajaribu kusema kwamba udhaifu wa kimwili aliokuwa nao Kristo ulikuwa hauna athari zo zote dhidi ya asili yake ya kiroho? Je, isingekuwa ni kweli kwamba Kristo angekuwa na mwelekeo mkubwa sana wa kukata tamaa au kukasirika wakati mwili wake ulipokuwa umechoka sana? Kama hayo ni kweli, basi, Kristo angekuwa na mielekeo inayomsukuma kwenda dhambini katika asili yake ya kimaadili [kimwili] au ile ya kiroho.

(2)
Inadokeza Kuwapo Kwa Asili ya Mseto
Ambayo Hakuwa Nayo Adamu,
Wala Wale Walioishi Baada Yake

Pakiwa hapana mchanganyiko kama huo unaojulikana miongoni mwa wanadamu, basi, asili hiyo tofauti kabisa isingeweza hata kidogo kuitwa “asili ya kibinadamu.” Ingegongana vibaya sana na matakwa ya Biblia yanayosema kwamba Kristo “ilimpasa KUFANANISHWA NA NDUGU ZAKE KATIKA MAMBO YOTE” (Waebrania 2:17). Hakuna mtu ye yote ambaye angeendelea kung’ang’ania kusema kwamba mchanganyiko kama huo wa asili isiyoanguka na ile iliyoanguka dhambini ungeweza kufanana na ndugu zake “katika mambo yote!” Ungekuwa haufanani na “ndugu zake” kabla ya lile Anguko kama yeye angekuwa na asili ya kimwili iliyoanguka dhambini, wala usingekuwa sawa na “ndugu zake” baada ya Anguko lile endapo yeye angekuwa na asili ya kiroho isiyoanguka dhambini. Ni “ndugu zake” wengine gani, basi, waliobaki? Mantiki inatulazimisha kukiri mwishowe kwamba kama asili yake “katika mambo yote … [i]lifanana” na ndugu zake, basi, ingetakiwa baadhi ya ndugu zake waonyeshwe ambao walikuwa na asili ya kiroho isiyoanguka dhambini pamoja na asili ya kimwili iliyoanguka dhambini. Kama hakuna ndugu yake kama huyo awezaye kupatikana, basi, kwa vyo vyote vile [Kristo] ingempasa kuwa na asili [mwili] ile ya kibinadamu ili “katika mambo yote [apate] kufanana” na Adamu baada ya Anguko lake. Kufanya vinginevyo kutakuwa ni kuyakataa maneno yaliyo wazi ya Maandiko au kuikataa mantiki hiyo rahisi.

(3)
Ingefutilia Mbali Kuwapo Kwa
Uwezekano Wo Wote Kwa Kristo
Kuweza Ku“jaribiwa Sawasawa Na Sisi
Katika Mambo Yote.”

(Waebrania 4:15)

Linaonekana kama ni jambo lisilowazika kusema kwamba ile asili takatifu ya Adamu aliyokuwa nayo kabla ya Anguko lake ingeweza kujaribiwa katika mambo yote sawasawa na sisi tunavyojaribiwa. Yeye hakuwa na kitu cho chote ndani yake kilichovutwa na majaribu ya aina yo yote, na hakika hakuna mtu ye yote atakayesema kwa kusisitiza kwamba asili zetu hizi zilizoanguka dhambini hazijaribiwi kwa nguvu sana ndani yetu. **Theolojia safi haipigani vita dhidi ya akili inayotumia mantiki**. Lo lote lile tunaloliamini juu ya jambo hili ni lazima liafikiane na maneno ya Biblia yanayoeleweka wazi. Kama Yesu alijaribiwa katika mambo yote "sawasawa na sisi," basi, majaribu hayo yasingeweza kuwa katika nyanja ya kimwili peke yake. Sehemu kubwa sana ya majaribu yetu hutokana na asili [miili] zetu dhaifu kiroho na kimaadili [kimwili]. Kama chimbuko hilo la majaribu yetu yenye nguvu kabisa lilikuwa halimo ndani ya Yesu, basi, asingeweza kabisa kujaribiwa katika mambo yote "sawasawa na sisi." Ingekuwa ni kujipinga wenyewe kutoa maoni ya kitu kama hicho.

Hebu sasa na tuangalie kwa kifupi ushahidi wa Biblia unaounga mkono mtazamo huo usemao kwamba Kristo alitwaa asili [mwili] ya Adamu baada ya lile Anguko. Sura ya pili ya Waebrania ina mambo mengi juu ya somo hili. Hebu yatafakari maneno haya: "Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye [Kristo] naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo…. Hivyo ilimpasa kufananishwa na ndugu zake katika mambo yote, apate kuwa kuhani mkuu mwenye rehema [huruma], mwaminifu katika mambo ya Mungu" (Waebrania 2:14-17).

Kifungu hiki ni kimojawapo kinachopatikana katika Biblia ambacho kinatilia mkazo sana na kutoa ufafanuzi. Yametumika maneno yaliyochanganywa pamoja ambayo hayaachi shaka lo lote kabisa kuhusu kile kinachoongelewa hapo. Neno lo lote kati ya hayo lingeweza kueleza wazo lililotolewa hapo ambalo linaeleweka wazi.

Kwa mfano:

Alishiriki *yayo hayo* au
Yeye *naye* alishiriki yayo hayo
Yeye *mwenyewe* alishiriki yayo hayo
Yeye *vivyo hivyo* alishiriki yayo hayo
Ilimpasa kufananishwa na ndugu zake *katika mambo yote*

Kwa nini Mungu alichagua kutoa shinikizo hilo la mambo matano na kuyaweka maneno yote hayo pamoja katika mkao mmoja wa Maandiko hayo? Karibu yote yanasikika kama ni marudio. "Yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo." Hakika sababu imo katika maana ya pekee ya ile kweli inayoelezwa hapo. Mungu hakutaka kuacha mashaka yo yote yanayoendelea kuwapo daima kuhusu ile asili [mwili] aliyokuwa nayo yule Mwana-Kondoo aliyechinjwa. Kukosa kuelewa ko kote kule ambako kungekuwako hapo kungeweza kukitupa kivuli chake juu ya ule Mpango mzima wa Wokovu. Kungetoa changamoto dhidi ya uhalali wa kifo chake Kristo ambacho alikufa badala yetu pale msalabani, na dhidi ya utoshelevu wa haki yake ambayo anatuhesabia sisi.

Hivi yawezekanaje kwa mtu ye yote kukosa kuelewa vizuri maana ya lugha halisi iliyotumika katika mafungu hayo? Jibu lake ni dhahiri. **Shetani anaichukia sana kweli hiyo**. Ni kielelezo dhahiri kinachoifichua hila yake idanganyayo ambayo kwayo yeye anaweza kulichukua fungu ambalo maana yake inaeleweka wazi kabisa na kuitia giza maana yake. Pia ni mfano unaoshangaza sana wa uwezo wa akili ya mwanadamu inayomfanya akiamini kile tu anachotaka kukiamini.

Mimi nawasilisha maoni yangu kwamba endapo Mungu angekuwa ametumia njia kumi au ishirini hivi kusema kitu kile kile kimoja, bado kingekataliwa tu na wale wasiotaka kukiamini. Je! hivi ingeweza kuwaletea ushawishi mwingi zaidi wa kuamini kama yangeongezwa maneno na vifungu vya maneno vya ziada? Kwa mfano, "Yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo katika mambo yote." Ingekuwa ni kazi bure kuongeza vivumishi (adjectives) vingi na ufasaha wa kusema (rhetoric), maana jambo hilo lisingeweza kulifanya suala hili kueleweka kwa wazi zaidi kama vile linavyoeleweka sasa.

Angalia kwa makini kifungu kile cha maneno kisemacho "alishiriki yayo hayo." Hivi kina maana gani? Yayo hayo ni yepi? Fungu lililotangulia linatoa jibu. Anafanana na watoto wanaozaliwa kwa mwili na damu. Kwa kielelezo hicho, mwandishi huyo wa Biblia anafunga mlango wa kuwapo kwa uwezekano wo wote wa kukisia-kisia tu juu ya asili [mwili] ya kibinadamu aliyokuwa nayo Yesu. Hakuna jambo lo lote zaidi ya hilo ambalo lingeweza kuwasadikisha. Kwa kuwa hakuna watoto wo wote waliozaliwa katika dunia hii kabla Adamu na Hawa hawajatenda dhambi, basi, ni hakika kwamba kila mtoto aliyeshiriki mwili na damu ni lazima alishiriki asili [mwili] ya Adamu aliyokuwa nayo baada ya kuanguka dhambini. Kwa hiyo mwandishi wa kitabu hiki cha Waebrania alipoandika kwamba Yesu "alishiriki YAYO HAYO" na kwamba "ilimpasa kufananishwa na ndugu zake KATIKA MAMBO YOTE" alikuwa ametoa dai ambalo haliwezi kukanushwa. Ni kwa kutoa tu uthibitisho unaoonyesha kwamba baadhi ya watoto walizaliwa kwa mwili na damu pasipo kuwa na asili ile ya dhambi, ndipo, kwa kutumia mantiki, mtu ye yote angeweza kupinga kwamba Kristo hakuwa na asili [mwili] ile aliyokuwa nayo Adamu baada ya Anguko. Fungu lile lile kabisa linatangaza kwamba yeye naye alishiriki asili [mwili] ile ile kama watoto wengine wote waliozaliwa [humu duniani] ili "apate kuwa kuhani mkuu mwenye rehema [huruma], mwaminifu … ili afanye suluhu [upatanisho] kwa dhambi za watu wake." Kwa njia hiyo tu [ya kufanana na ndugu zake kimwili] yeye angeweza kujipatia sifa ya kuwa mwakilishi anayefaa wa familia ya kibinadamu mbele za Baba yake [Ebr. 4:14-16].

Mtu fulani mmoja anaweza kubisha na kusema kwamba Kristo angeweza kufanya lo lote alilotaka kufanya bila kuwekewa mipaka ya aina yo yote. Naam, angeweza kufanya vile. Angeweza kuchagua kutenda dhambi, lakini katu yeye hakufanya hivyo! Angekuwa ameweza kujiokoa mwenyewe ili asipatwe na maumivu ya miiba na misumari ile, lakini katu yeye hakufanya vile! Mungu na ashukuriwe, kwa kuwa yeye hakufanya mambo yo yote kama hayo, bali yeye "alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti [kwa zile Amri Kumi – Yn. 15:10; Zab. 40:8]; naam, mauti ya msalaba." Ni Mwokozi wa jinsi gani huyo!

ANGALIA: Maneno na mafungu yaliyo katika mabano haya [ ] yameongezwa kwa ajili ya ufafanuzi na kujifunza zaidi. Yasinukuliwe.